



12/06/2023

Mzazi wa :

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE.

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika Shule ya Sekondari Sengerema kwa mwaka wa Masomo 2023/2024. Anapaswa kufika Shuleni tarehe 13/08/2023 kabla ya saa 11: 00 jioni. Shule ipo kata ya Mwabaluhi Wilaya ya Sengerema – Mwanza umbali wa kilometa 3.2 kutoka stendi kuu ya mabasi ya mjini Sengerema. Anaweza kufika Shuleni kwa teksu Tsh. 5,000/= au pikipiki kwa Tsh. 2,000/=

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.0 MICHANGO YA SHULE

s/n	Aina ya michango	Kiasi
1.	Mchango wa uendeshaji wa shule	65,000/=
2.	Tahadhari	5,000/=
3.	Nembo	5,000/=
4.	Kitambulisho cha shule	5,000/=
	Jumla	80,000/=

1.1 Bima ya Afya:

Jukumu la matibabu ni la mzazi/mlezi, unashauriwa kumlipia mtoto wako Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) ambapo shule itawaunganisha na ofisi za NHIF mkoa wa Mwanza kupata bima hizo. Kila mwanafunzi ni lazima aje na Bima ya Afya ya NHIF. Kwa wale wasio kuwa nazo waje na shilingi 50,400/= ili wapatiwe bima hizo na ofisi za bima (NHIF) ya mkoa wa Mwanza. Malipo hayo ya bima ni kwa mwaka.

Fedha za michango ya Shule zilipwe kwenye akaunti Na. 31601100001 NMB tawi lolote Tanzania Jina: Sengerema Secondary School Fund Account.

2.1 "Shule haipokei fedha taslimu". Fedha zote zilipwe kupitia Bank ya NMB tawi lolote.

Kwa kutumia namba za Akaunti husika na stakabadhi za malipo (Bank pay in slips) zenye jina la mwanafunzi ziletwe Shuleni siku ya kuripoti. **Mwanafunzi hatapokelewa Shuleni endapo hatakamilisha malipo yote ya fedha kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo juu.**

2.2 Tarehe ya kufungua Shule imeoneshwa hapo juu, mwanao akichelewa kuripoti Shuleni ndani ya siku kumi na nne atakuwa amepoteza nafasi yake.

2.3 Aje na photocopy ya cheti cha kuzaliwa na photocopy ya result slip ya matokeo ya kidato cha NNE.

2.4 Mwanafunzi na Mzazi / Mlezi wakumbuke kusoma kwa makini / kujaza na kusaini fomu ya Sheria za Shule na kukiri kusoma kwa bidii na kufaulu mitihani yetu na fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano endapo kutatokea dhalura.

2.5 Fomu ya uchunguzi wa afya ya mwanafunzi iliyojazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali iwasilishwe siku ya kuripoti Shuleni.

2.6 Nguo za nyumbani haziruhusiwi, Mwanafunzi atavaa sare za Shule muda wote awapo Shuleni. Pindi anapokuja Shuleni kuripoti awe amevaa Suruali ya rangi nyeusi ya kitambaa na shati nyeupe yenye mikono mirefu isiyokuwa na vishikizo vya chuma.

2.7 Kila Mzazi / Mlezi anapaswa kugharamia usafiri wa mwanee kuja Shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.

2.8 Mzazi / Mlezi epuka matapeli wanaopiga simu kwa "kisingizio cha ugonjwa. Shule yetu ina utaratibu wa kumjulisha mzazi pindi panapotokea tatizo kwa mwanao.

3.0 SARE YA SHULE

